# Alasiri Online

www.ippmedia.com

ISSN 0856 Na. 001 Jumatatu Machi 4, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-

## UNENE WAMTESA KAJALA



## MPOTO AMSHIKA SIKIO DIAMOND

# OMMY DIMPOZ ASAMEHE



Na Mary Kadoke

OMMY Dimpoz amesema kuwa hana kinyongo na msanii Steven Nyerere, licha ya kile kilichoelezwa kama utabiri wa Stephen Nyerere kuwa hataimba tena baada ya kuugua kansa ya koo.

Akizungumza na Alasiri Online, Dimpoz amesema kuwa yeye moyo wake ni mweupe na hana tatizo, chuki, au kinyongo na msanii huyo wa maigizo kwa kile alichokifanya siku za nyuma.

"Urafiki wangu na Stephen Nyerere ni wa siku nyingi hatuwezi kugombana," amesema.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo, udugu hazina yetu," amemalizia.

Hivi karibuni baada ya Nyerere kufanyiwa mahojiano na Times FM kuhusu afya ya msanii mwenzake Ommy Dimpoz, alisema haoni matumaini ya msanii huyo kurudi kwenye game kutokana na kuathirika kwa koo lake.

"Ommy hataimba tena," alisema.

Aidha baada ya kauli hiyo ni kama alichochea watu hasa team Ommy kumshambulia mitandaoni alipopona na kuachia ngoma yake mpya, 'Ni Wewe' yenye watazamaji milioni 1.6 katika mtandao wa YouTube mpaka sasa.

Hivi huyu ni Mungu kumtabiria mwenzake kuwa hataimba? Anataka nini huyu michango au? Ni baadhi ya maswali yaliyoibuliwa na mashabiki katika mtandao wa Instagram katika mahojiano ya Times na Nyerere.

Dimpoz alifanyiwa upasuaji nchini Afrika Kusini baada ya kuugua kansa ya koo Julai mwaka jana.

# MSONDO KUPAGAWISHA MIKOANI



Na Anaeli Mbise

BENDI kongwe ya muziki wa dansi nchini ya Msondo Ngoma inatarajia kuanza safari za mikoani kwa ajili ya kutoa burudani kwa mashabiki.

Akizungumza na Alasiri Online, kiongozi wa bendi hiyo Said Mabera, amesema kuwa lengo kubwa la kwenda mikoani ni ili kuwarudishia mashabiki wao burudani ambayo wamekuwa wakiikosa kwa siku nyingi.

"Kwa kuanza tunaanzia Morogoro, Tanga na ukanda wa kaskazini hii ni kuwapa fursa mashabiki wetu wajue baba ya muziki tupo na tunaendelea kuwapa raha mashabiki," amesema Mabera.

Mabera ameongeza kuwa wanamuziki wote wa Msondo wako vizuri kwa ajili ya matamasha hayo ambayo yaanza katikati mwa mwezi huu.

Kwa upande wake mmoja wa wapiga kinanda wa bendi hiyo, Ridhiwani Pangamawe maarufu kama Tottoo amesema kuwa mashabiki wa mikoa ambayo watapita wasikose maana itakuwa ni burudani ya aina yake.

Msondo ngoma imewahi kutamba na nyimbo kama vile Tabu, Harusi ya Kibene, Ndoa Ndoano, Kilio cha Mtu Mzima, Piga Ua Talaka Utatoa, Jesca, pamoja na Kalunde.



# MPOTO AMSHIKA SIKIO DIAMOND

**Na Mary Kadoke**

MRISHO Mpoto amemshauri Diamond Platnumz kusahau yaliyopita kati yake na marehemu Ruge Mutahaba na badala yake kushiriki na wasanii wenzake msiba huo.

Kama kaka amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akimfahamisha kuhusu msiba huo na kusisitiza kuweka tofauti zao pembeni.

"Nassib Abdul nimekuita kwa jina lako la kuzaliwa mimi kama kaka yako unaeniheshimu na kunisikiliza nakuambia Ruge Mutahaba amefariki nakuomba njoo umzike nimemaliza," amesema.

Aidha Ney wa Mitego ambaye pia aliwahi kuwa karibu na Diamond amemueleza kuwa asitumie muda mwingi kufikiria ya duniani kwani ni ya muda.

"Sina zaidi cha kuongea, lakini cha kumuambia ni kwamba duniani tunapita," amesema.

Aidha pamoja na Alasiri Online kufanya juhudi za kumsaka Diamond ili kujua msimamo wake juu ya hili, hazikuzaa matunda.

Mgogoro kati ya Diamond na marehemu Ruge umekuwa wa muda tangu yazuke madai ya Diamond kudhulumiwa pale anapofanya kazi mbalimbali na shujaa huyo aliyetutangulia mbele ya haki.

Dalili za kutofautiana kwa wawili hawa zilipigiwa mstari pale Diamond alipoamua kufungua kampuni yake ya redio Wasafi FM, televishenI Wasafi Tv na tamasha la muziki 'Wasafi Festival' kurahisisha utendaji wa kazi zake.

Hata hivyo, pamoja na minong'ono kuendelea kuhusu tuhuma hizo, marehemu Ruge kupitia mahojiano aliyowahi kufanya na Clouds 360 mwaka jana alisema hakuwahi kuwadhulumu wale wanaodai aliwahi kuwafanyia hivyo.

Aliamini kuwa ana mchango mkubwa kwa hapo walipofika na kama kuna malalamiko wanayotoa wa kujibu ni Mungu kwani ndiye anayejua ukweli wote.

Ruge alifariki Februari 26 akiwa anapata matibabu Afrika Kusini, baada ya kusumbuliwa na figo tangu Septemba mwaka jana.



# Unene wamtesa Kajala

**Na Anaeli Mbise**

MREMBO kutoka Bongo 'Movies' Kajala Masanja amefunguka kuwa kati ya vitu ambavyo anavichukia kwa sasa ni pamoja na mwili kuwa na unene uliopitiliza

Akizungumza na Alasiri Online, amesema ubonge wake kwa sasa umefikia kiasi cha kumnyima raha kutokana na nguo nyingi kushindwa kuzivaa kwa sababu hazimpiti mwilini.

"Jamani huu mwili mpaka nahofia naweza kupata presha au gonjwa lolote linalotokana na kunenepa sana maana hata mazoezi naona sasa yamedunda, najitahidi kupambana ili niweze kurudi kama zamani," amesema Kajala.

Aidha Kajala ameongeza kuwa atafanya mazoezi ya kutosha ili kuurejesha mwili uwe kama zamani.

Msanii huyo amecheza filamu kama vile Kigodoro, House Boy, Vita Baridi, You and Me pamoja na Devils Kingdom.

# Kumbe wanawake noma!



Na Mary Kadoke

MUIGIZAJI Yussuf Mlela ataja ulevi na wanawake kama mambo yaliyompoteza kwenye ramani ya kuigiza.

Akizungumza na Alasiri Online amesema kwa muda amekuwa akipata lawama kutoka kwa watu wake wa karibu kuhusu muenendo wake na baada ya kuyatafari akafanya maamuzi ya kubadilika.

"Kwa sasa nimeacha kabisa mambo ya pombe na wanawake unajua vimeniponza sana, kila mara nilikuwa nagombana na bi mkubwa na kuona kama ananibana vile," amesema.

"Sasa majukumu yananibana nasomesha hivyo nalazimika kubadili mfumo mzima wa maisha yangu," amesema.

Kazi zilizomtambulisha ni pamoja na I Know You na April Fools.

# Wasanii na siasa




Na Anaeli Mbise

BENDI ya muziki wa dansi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, imepata shavu la kutangaza Chama Cha Mapinduzi (CCM), kujiandaa na chaguzi mbalimbali.

Akizungumza na Alasiri Online, mkurugenzi wa bendi hiyo Killer David amesema amepewa jukumu la kutunga wimbo unazungumzia mazuri yaliyofanywa na CCM mkoani humo.

"Tunajiandaa kwenda kurekodi wimbo ambao tumetunga kwa ajili ya chama, tumepewa jukumu la kutangaza Ilani ya chama katika mkoa wa Morogoro," amesema Killer.

Aidha Killer ameongeza kuwa sababu ya kufanya kazi na chama hicho kikongwe ni kwa ajili pia ya biashara ili kujipatia kipato kupitia njia ya muziki.

Mbali na Waluguru Original, bendi nyingine inayoimba nyimbo za kusifia CCM ni pamoja na Tanzania One Theartre (TOT), ikiongozwa na malkia wa mipasho Khadija Kopa katika safu ya waimbaji.